

TANGAZO KWA UMMA

**MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI YA
HUDUMA ZA MAJI KUTOKA MAMILAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA
MJI WA MUGUMU (“MUGUMU WSSA”) KWA MWAKA 2019/20 – 2021/22**

Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-013

Mnamo tarehe 2 Mei 2019, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mji wa Mugumu (Mugumu WSSA) la kutaka kurekebisha bei za huduma za majisafi kwa mwaka 2019/20 hadi 2021/22. Jedwali hapa chini linaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

Jedwali: Bei za Maji za sasa na zinazopendekezwa (Shilingi kwa mita moja ya ujazo)

Kundi la Wateja	Bei za Sasa	Bei Zilizopendekezwa					
		2018/19	Badiliko	2019/20	Badiliko	2020/21	Badiliko
Majumbani	540	122.2%	1,200	8.3%	1,300	7.7%	1,400
Taasisi	550	136.4%	1,300	3.8%	1,350	3.7%	1,400
Biashara	560	150.0%	1,400	7.1%	1,500	6.7%	1,600
Magati	560	150.0%	1,400	7.1%	1,500	6.7%	1,600

Kwa mujibu wa wasilisho la Mamlaka ya Maji Mugumu, bei zinazopendekezwa zitaiwezesha Mamlaka kupata mapato ya kutosha kumudu ongezeko la gharama za uendeshaji na matengenezo. Aidha, Mamlaka ya maji Mugumu imebainisha kuwa mabadiliko ya bei yanayopendekezwa yataiwezesha Mamlaka kumudu gharama za uendeshaji zilizoongezeka, kuboresha huduma za maji safi ikiwa ni pamoja na kuongeza mtandao wa majisafi na kufanya uwekezaji wa miundombinu ya maji kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma ya maji safi katika mji wa Mugumu.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Ijumaa, tarehe 28 Juni 2019, katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya Serengeti, Mjini Mugumu** kuanzia saa **4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu kabla ya tarehe **4 Julai 2019 saa 10.00 jioni**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana Ofisi za UWURA Kanda ya Ziwa, **GHOROFA YA NNE, JENGO LA PPF, MTAA WA KENYATTA, S.L.P 2069 MWANZA** au **Ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mugumu** zilizopo mjini Mugumu.

**Imetolewa na:
Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)
12 Junii 2019**